

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu Na: 2602320 / 2600891  
Fax Na: 2602320 / 2602176  
Email: [dedsongea@yahoo.com](mailto:dedsongea@yahoo.com)

S. L. P. 995,  
SONGEA.



Kumb: Na: DED/SO/D.30/320/8

24.04.2018

## Kwa Yeyote Anayehusika.

### YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA NKUSU THEO SUGAR LTD

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Halmashauri ya Wilaya ya Songea inakamilisha taratibu za makubaliano ya awali kati yake na Kampuni ya Nkusu Theo Sugar Ltd ya S. L. P. 2406, Mbeya ili kuwekeza katika kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari katika Kijiji cha Nakawale, Kata ya Muhukuru baada ya kukaribishwa na mpango wa uwekezaji wa Kampuni hii wa dola za kimarekani 80,000,000.00, kupokelewa vizuri na wananchi wa eneo la mradi, Halmashauri na Mkoa kwa ujumla.

Aidha, taratibu mbalimbali zimekwishafanyika ikiwa ni pamoja na kupata ridhaa ya wananchi ya kutwaliwa kwa ardhi ili itumike katika uwekezaji huo. Baada ya ridhaa ya wananchi, Kamati ya kugawa ardhi ya Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Songea, nyaraka mbalimbali za uhawilishaji zimeshawasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi kwa hatua zinazofuata ambapo baada ya hatua hizo kukamilika upimaji kamili na umilikishaji utafanyika kwa mujibu wa sheria.

Hivyo, Halmashauri inaitambua Kampuni ya Nkusu Theo Sugar Ltd kama miongoni mwa makampuni yanayoendelea na taratibu za uwekezaji katika Halmashauri. Pia kwa vile tunatambua Kampuni ina mambo na taratibu nyingine nyingi za kukamilisha ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uwekezaji huu, Halmashauri inapenda kuitambulisha na kuziomba Taasisi na

Mamlaka nyingine zote zinazoweza kuhusika kuwapokea na kutoa ushirikiano au msaada utakaohitajika.

Barua hii inafuta barua yenye Kumbukumbu Namba DED/SO/D.30/320/7 ya tarehe 23.04.2018.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha na ramani ya upimaji wa awali ya shamba la uwekezaji lenye ukubwa wa ekari 35,398.

Natanguliza shukrani.



*Simon M. Bulenganija*  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
SONGEA



Nakala: Mhe. Waziri wa Viwanda na Biashara,  
S. L. P. 9503,  
**DAR ES SALAAM.**

“ Mhe. Mkuu wa Mkoa,  
S. L. P. 74,  
**RUVUMA.** - Kwa taarifa.

“ Katibu Tawala (M)  
S. L. P. 74,  
**RUVUMA.**

“ Mkuu wa Wilaya,  
S. L. P. 1,  
**SONGEA.** - Kwa taarifa.

“ Mhe. Mbunge,  
Jimbo la Peramiho,  
S. L. P. 1,  
**PERMIHO.** - Kwa taarifa.

**PROPOSED SURVEY PLAN OF FARM NO.....AT NAKAWALE VILLAGE  
SONGEA DISTRICT COUNCIL**

